



Mswada wa Haki na Majukumu ya Mgonjwa

Vituo vya Afya vya Jamii vya Burlington (CHCB) vina furaha kukuhudumia kama mgonjwa wetu. Tumejitolea kukutibu kwa uangalifu na kwa heshima, huku tukiheshimu haki zako za kisheria, na kufanya kazi ili kutimiza mahitaji yako ya huduma ya afya. Ili kuifanya huduma hii iweze kutufainisha sote na inayofurahiwa, na ili kuwasaidia wafanyakazi wetu wenye ujuzi na wanaojali kukutibu, tumeorodhesha haki na majukumu yako kama mgonjwa wa CHCB.




617 Riverside Avenue
Burlington, VT 05401

www.chcb.org



Mswada wa Haki na Majukumu ya Mgonjwa





Una haki ya:

- Kushiriki katika matibabu ya huduma yako ya afya.
- Kujua majina ya watu wanaokuhudumia.
- Kutibiwa kwa heshima na uadilifu katika mazingira salama na ya faragha.
- Kufahamishwa kuhusu ugonjwa na matibabu yako, pamoja na chaguo za huduma yako.
- Kuomba kubadilishiwa watoa huduma ya matibabu.
- Kupata maoni mengine kuhusu ugonjwa au matibabu yako.
- Faragha ya rekodi zako za afya.
- Imani yako ya kitamaduni, kijamii, kiroho na kibinafsi kuheshimiwa.
- Kufahamu kuhusu mahitaji ya kisheria ya kuripoti.
- Kupewa mkalimani ikiwa una ugumu wowote wa kusikia, kuongea au kuelewa Kiingereza.
- Kuomba malazi maalum na yanayofaa ikiwa una ulemavu.
- Kuomba msaada wa wosia wa kuishi au huduma za wakili wa huduma ya afya.
- Kukataa matibabu na huduma kama invyoruhusiwa na sheria.
- Kujua gharama ya huduma yako na njia unazolipia huduma yako.
- Kuongea na meneja wa CHCB ikiwa una malalamiko.
- Kuibua hoja zako kwa kuandika barua kwa Patient Relations Committee, 617 Riverside Avenue, Burlington, VT 05401 or by visiting www.chcb.org na kwenda kwenye ukurasa wa Wasiliana Nasi.
- Kuibua hoja kuhusu kufuata sheria kwa kumpigia simu Afisa wetu wa Kutii, nambari ya simu (802) 264-8152.

CHCB Inakubali:

- Kutoa huduma ya afya kwa mtu yeyote anayehitaji licha ya uwezo wake wa kulipa.
- Kutoa kipunguzo cha ada kwa wagonjwa wasio na bima na wasio na bima ya kutosha wanaopata chini ya asilimia 200 ya Kiwango cha Umasikini cha Serikali na wale ambao hawana makao.
- Kukufahamisha kuhusu huduma tunazotoa.
- Kukupa huduma kwa wakati unaofaa, kulingana na uwezo wa rasilimali zetu.
- Kutoa chaguo wazi za uaguzi na matibabu tukiweza, na kuwa wazi na wewe wakati hatujui au hatuna uhakika.
- Kutoa masharti wazi kuhusiana na huduma tutakayokupa na matibabu ambayo hatuyashauri au ambayo hatuwezi kuyatekeleza.
- Kukudhamini wewe kama mgonjwa na mtu.



Una Haki ya:

- Kushiriki katika matibabu ya huduma yako ya afya.
- Kutupatia maelezo ili rekodi zako ziwe sahihi na kamili.
- Kutusaidia kupata nakala ya rekodi zako za afya kutoka kwa watoa huduma wako wa zamani ikihitajika.
- Kumwambia mtoa huduma wako wa afya kuhusu magonjwa na matatizo yako.
- Kuuliza maswali kuhusu ugonjwa au huduma yako.
- Kuwasili kwa miadi mapema kabla ya muda ulioratibiwa.
- Kughairi au kupanga upya miadi ili mtu mwingine apate nafasi hiyo.
- Kutumia dawa au vifaa vya kitabibu kama ilivyoagizwa na kwa ajili yako pekee.
- Kumfahamisha mtoa huduma ya matibabu ikiwa utakuwa mgonjwa zaidi au una madhara yasiotarajiwa yanayotokana na dawa.
- Kupiga simu angalau siku mbili mapema ili kuongezea dawa zako.
- Kuwaongelesha na kuwatendea kwa heshima wafanyakazi, wagonjwa na wageni wote.
- Kuheshimu faragha ya wagonjwa wengine.
- Kulipia bili yako kwa wakati unaofaa, au ikiwa una ugumu, kupanga mpango wa malipo kwa kupiga simu (802) 264-8126.
- Kuomba faida kwa kutembelea Huduma ya Msaada kwa Wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Riverside au kupiga simu kwa (802) 864-6309 na uombe uongee na mwakilishi wa kustahiki.